ABDALLAH YAKOBO,
LAMBO ESTATE,
S.L.P366,
**MOSHI.**
29/12/2023

MWENYEKITI WA BODI 04/01/2024

FONRWACIE LIMITED

LAMBO ESTATE

S.L.P 366

**MOSHI**

**YAH: <u>NOTICE YA KUBOMOA JENGO LANGU</u>.**

Rejea barua yako kwangu yenye Kumbukumbu namba FNW/CIE/LL/3/392 ya tarehe 20/12/2023 iliyo na kichwa cha habari "NOTICE YA KUBOMOA JENGO ULILOJENGA AU UNALOJENGA".

Kimsingi wewe sio msimamizi wa eneo la Evari 156 za sisi wananchi wa Lambo Estate tulizopewa na serikali tangu tarehe 25/10/2018 kupitia waziri mwenye dhamana ya ardhi ambapo kwa sasa serikali ipo kwenye hatua za mwisho kutupatia HATI MILIKI bila ya kuwepo zuio lolote la kuendeleza maeneo yetu.

Ninakukumbusha pia wewe ndiye kiini na msingi wa mgogoro uliokuwepo huku ukisahau kuwa ulisharidhia sisi wananchi wa Lambo Estate kupatiwa na serikali "makazi ya kudumu" katika mkutano wenu mkuu maalumu wa tarehe 16/12/2011

Kwa kuzingatia wewe kutokuwa msimamizi wa eneo langu la Ekari mbili (2) nililopewa na serikali, tambua NOTISI uliyonipa haina msingi na SITAIZINGATIA.

Aidha ninakushauri unayepaswa kusuguana naye ni serikali kupitia Wizara husika waliotwa kipande cha ekari 156 kutoka kwako na kutupatia sisi wananchi wa Lambo Estate kwa ajili ya makazi yatu ya kudumu na siyo vinginevyo.

Mwisho ninakuusia siyo busara kwako kuibua migogoro ya mara kwa mara isiyo na msingi wowote zaidi ya kuendekeza UKABILA na UBINAFSI usio na nafasi katika Taifa lenye kuzingatia haki na usawa.

Asante,

Wako

Yakobo
.......................................

ABDALLAH YAKOBO

**NAKALA:**

1. MRAJISI WA VYAMA VYA USHIRIKA
   TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA
   S.L.P 201
   DODOMA

2. MKUU WA MKOA KILIMANJARO

   S.L.P 3070

   MOSHI

3. MRAJISI MSAIDIDISI WA VYAMA VYA USHIRIKA MKOA WA KLIMANJARO
   S.L.P 3070
   MOSHI

4. MKUU WA WILAYA YA HAI

   S.L.P 10

   HAI

5. MKUU WA POLISI MKOA WA KILIMANJARO

6. MWENYEKITI WA KIJIJ CHA NSHARA

7. MKURUGENZI MTENDAJI-HALMASHAURI (W) HAI